BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI

Kikao cha Ishirini na Moja – Tarehe 06 Juni, 2018.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa Mwaka 2018/2019.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa Mwaka 2018/2019.

III. MASWALI:

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

99. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Mazingira halisi ya jiografia ya Kijiji cha Mkiawang'ombe, kunahitaji kuwepo kwa mkunga mzalishaji na upatikanaji wa maji katika kituo cha Afya kilichopo katika kijiji hicho. Kukosekana kwa mkunga kunapelekea wajawazito kusafirishwa masafa marefu na wakati mwengine kupelekea kufariki njiani ambapo wajawazito wawili walifariki kabla ya kufikishwa hospitali.

(a) Je, ni lini Wizara itampeleka Mkunga katika kituo cha Afya katika kijiji hicho na kumwekea mazingira bora ya kufanya kazi.

(b) Je, Ofisi yako itashirikiana vipi na Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati kulimaliza tatizo la maji linalokikabili kituo hicho cha Afya.

Wizara ya Fedha na Mipango

264. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango.

Kwa muda mrefu sasa tokea Hoteli ya Bwawani imeingia kwenye mpango wa kukodishwa na kujengwa upya, hakuna kinachoendelea. Kwa kuwa wananchi wanataka kujuwa kitu gani kinaendelea kwenye mtaji ule wa umma.

(a) Je, Serikali inawaeleza nini wananchi kuhusu kinachoendelea katika hoteli ya Bwawani.

(b) Kwanini imechukuwa muda mrefu kukamilisha mradi unaokusudiwa kufanyika.

(c) Je, Mwekezaji wa mradi unaotaka kufanyika bado anayo nia ya kuendelea.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

91. MHESHIMIWA HIDAYA ALI MAKAME (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Walimu Wakuu ni moja ya maafisa wa Wizara katika utawala wa skuli zetu hapa Zanzibar wakiwa na majukumu ya utawala, usimamizi wa skuli na kusomesha. Pamoja na Walimu Wakuu kuendelea kufanya makujumu hayo lakini bado inaonekana wana mzigo mkubwa wa kazi hizo kuzifanya kwa ufanisi yaani kuendesha shughuli za utawala wa skuli ambazo ni nyingi na wakati huo huo kusomesha wanafunzi.

(a) Kwanini Wizara haiweki mpango wa kuwapunguzia Walimu Wakuu majukumu ya kusomesha na badala yake wakabakia na majukumu ya Utawala na Usimamizi wa Skuli.

(b) Wizara inampango gani wa kuanzisha mfumo kwa skuli zetu wa kuwa na Mkuu wa skuli kwa majukumu ya utawala peke yake na Mwalimu Mkuu kwa majukumu ya kusimamia walimu na kusomesha kama wanavyofanya baadhi ya nchi jirani mfano Tanzania bara.

(c) Kwa kuwa majukumu hayo ya Walimu Wakuu ni mazito sana na inawafanya Walimu Wakuu wengi kutumia siku nzima wakiwa skuli tu, Wizara imejipanga vipi kuwaongezea posho la Mwalimu Mkuu kutoka kima cha sasa na kufikia angalau 100,000/=

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

148. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Uwanja wa ndege wa kimataifa wa Abeid Amani Karume ndiyo kielelezo cha nchi yetu kwa vile ndiyo mlango wa kuingilia, kumekuwa na tatizo la utaratibu usioeleweka wa kuegesha gari ambapo dereva anaweka gari yake anapewa adhabu bila kuwepo maelekezo ya wapi aegeshe.

(a) Je, sheria na taratibu za maegesho kwanini haziwekwi wazi badala yake wananchi wanasumbuliwa.

(b) Viwanja vya ndege vya Kimataifa vya wenzetu vinawekwa alama za maandishi na picha zikitoa maelekezo ya kila eneo la uwanja, kwanini uwanja wetu haufuati mpango kama huo.

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

217. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Katika msimu wa karafuu uliopita Serikali iliunda timu maalum ya kufanya tathmini katika mashamba ya mikarafuu ambayo yalikatwa eka na kugaiwa wananchi na kwa sababu wapo wananchi ambao waliipanda mikarafuu na kufikia kiwango cha kuchuma mikarafuu hiyo zaidi ya mara nne hadi tano.

(a) Je, kuna utaratibu gani kwa mtu aliyepanda mikarafuu kwenye shamba la Serikali ambayo imeshazidi miaka 12 kuendelea kushughulikia mikarafuu hiyo na Serikali kubaki kama ambavyo wapo watu wenye minazi au mikarafuu kwenye shamba ya mtu mwengine lakini ardhi sio yake.

(b) Je, mashamba mangapi yaliyobainika kwa wananchi waliopanda mikarafuu na Serikali inatoa wito gani kwa wananchi waliokuwa na mashamba ya Serikali ambayo yalikodishwa katika msimu uliopita kwa kuyaendeleza na kuilinda dhidi ya vitendo vya hujuma, wizi na wanaokata kuni.

Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

172. MHESHIMIWA ASHA ABDALLA MUSSA (Jimbo la Kiwengwa) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

Kwa kuwa wananchi wa kijiji cha Kipandoni na Kiwengwa bado wanaendelea kupata changamoto ya maji safi na salama na Waziri katika kikao cha Baraza aliwahi kuniahidi

kuwa changamoto hiyo itaondoka katika kipindi kifupi na wamo mbioni kutafuta fedha kwa wawekezaji ili kukamilisha mradi huo.

(a) Je, ni lini suala hili litatatuka.

(b) Je, Wizara imekusanya kiasi gani kwa ajili ya kukamilisha mradi huo.

(c) Je, Wizara ina mpango gani mbadala wa kuhakikisha wananchi hawa wanapata maji safi na salama hadi pale mradi utakapo kamilika

Wizara ya Biashara na Viwanda:

78. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Viwanda:

Wananchi wa jimbo la Paje wamekuwa wakiunga mkono juhudu za Serikali za kuimarisha zao la mwani kibishara, hata hivyo juhudi hizo zinaonekana kutofanikiwa kwa kuwa bei ya mwani ipo chini sana na inawavunja moyo wananchi wa Paje. Kwa kuwa kuna ahadi ya Serikali ya kuzitaka Wizara zote zinazohusika kukaa pamoja kuandaa mazingira ya kuimarisha bei ya mwani.

Je, kuna mpango gani Wizara imeuweka pamoja na hizo Wizara nyengine kuhakikisha kuwa bei ya mwani inaongezwa ili wakulima waweze kuinuwa vipato na hali zao za maisha.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa mwaka 2018/2019.

Zanzibar,
06 Juni, 2018.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.